

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA KUMI NA TANO**

24 APRILI, 2019



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA TANO – TAREHE 24 APRILI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

#### **122. MHESHIMIWA YUSSUF HAJI KHAMIS (NUNGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imeongeza idadi ya Majimbo ya uwakilishi kutoka 50 hadi 54, kabla ya ongezeko hilo Majimbo ya uwakilishi na Ubunge yalikuwa sawa kwa ukubwa, mipaka na idadi ya wapiga kura. Ongezeko hili limefanya Majimbo mawili ya uwakilishi kufanywa Jimbo moja la Ubunge:-

Je, ni lini Tume ya Taifa ya Uchaguzi itafanya uhakiki wa Majimbo ya Ubunge Zanzibar.

## **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

### **123. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Madiwani nchini wanafanya kazi kubwa sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea posho na mishahara au maslahi yao.

### **124. MHESHIMIWA JOSEPH LEONARD HAULE (MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Jimbo la Mikumi lina uhaba mkubwa wa Vituo vya Afya na hata pale ambapo kuna Kituo basi dawa na Wataalamu ni tatizo:-

Je, Serikali imejipanga vipi kutatua tatizo hilo sugu la uhaba wa Vituo vya Afya na dawa.



**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO:**

**125. MHESHIMIWA OMAR ABDALLAH KIGODA  
(HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi,  
Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni nini hatma ya kipande cha barabara ya  
Handeni-Mziha ambacho Serikali iliahidi  
kwamba Mkandarasi akishalipwa ujenzi  
utaanza; hasa ikizingatiwa kuwa barabara hiyo  
inaunganisha Mikoa miwili.

**126. MHESHIMIWA KHADIJA NASSIR ALI  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi,  
Uchukuzi na Mawasiliano:- Kwa kuwa Serikali  
ya Awamu ya Tano inaendelea na zoezi la  
kununua ndege:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka  
kuhakikisha kuwa ndege hizo zinakwenda kila  
Mkoa wenye Kiwanja cha Ndege pamoja na  
nchi jirani ili kusaidia kushusha gharama za  
usafiri.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **127. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini kiwanda cha Saruji cha Dangote kitapewa gesi asilia na TPDC.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **128. MHESHIMIWA MATTAR ALI SALUM (SHAURIMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Jeshi la Polisi lipo kwa mujibu wa Sheria na hupaswa kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria za nchi. Jeshi la Polisi linapowakamata baadhi ya watu huamuru wawekwe ndani zaidi ya saa 24 na kusababisha usumbufu mkubwa:-

Je, ni kesi zipi Mtuhumiwa anapaswa kuwekwa ndani chini ya saa 24.

**129. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

(a) Je, ni Wizara ipi inayowajibika kukusanya fedha za VIZA na kusimamia utoaji wa VIZA hizo;

(b) Je, kuna mgao wowote kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Uwanja wake wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Karume.

**WIZARA YA KILIMO:**

**130. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Pembejeo za kilimo ni ghali sana hivyo Wakulima wengi hushindwa kununua na kusababisha kupata mavuno haba:-

Je, Serikali ipo tayari kupunguza au kuweka bei elekezi iliyo nafuu kwa Mkulima ili aweze kupata pembejeo za dawa, mbolea na zana za kilimo.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **131. MHESHIMIWA DKT. PUDENCIANA WILFRED KIKWEMBE (KAVUU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua za kimkakati kuhakikisha kwamba migogoro kati ya Wafugaji na Wananchi wanaoishi pembezoni mwa mbuga za wanyama inakwisha kabisa:-

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA  
24 APRILI, 2019**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**